

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA APOKEA MWENGE WA UHURU.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Paul Makonda leo July 07 amepokea Mwenge wa Uhuru uliowasili Asubuhi ya leo Uwanja wa ndege wa Mwalimu Nyerere ukitokea Mkoa wa Kusini Pemba na kuukabidhi kwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala Bi. Sophia Mjema kwaajili ya kuanza shughuli ya uzinduzi wa miradi ya maendeleo.

RC Makonda amesema Mwenge wa Uhuru utakuwa Jijini Dar es salaam kwa Muda wa siku Tano ambapo utazindua na kuweka mawe ya msingi kwenye miradi 38 yenye thamani ya Shilingi Billion 33.4.

Aidha RC Makonda amesema katika miradi itakayozinduliwa kupitia mbio za mwenge, miradi 16 itazinduliwa, Miradi 14 itawekewa mawe ya msingi na Miradi 8 itatembelewa.

Mwenge wa Uhuru umeanza kwa kukimbizwa Wilaya ya Ilala na baada ya hapo utaenda Wilaya za Kigamboni, Kinondoni, Ubungo na kumalizia na Wilaya ya Temeke.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

07/07/2018

